MAGAZETI -NOVEMBA 16, 2026

1. NIPASHE NOV. 16, 2026



CamScanner

Nipashe MWANGA WA JAMII
Jumatatu Novemba 16, 2026

MAADILI

Tanzania yaweka msimamo mapenzi ya jinsia moja

Na Mwandishi Wetu,
GENEVA 0715086344
WhatsAPP SMS

TANZANIA imesema haikubaliani na mapendekezo ya kuhalalisha mapenzi ya jinsia moja 'ushoga' na kuondoa adhabu kwa makosa ya kujamiiana kinyume na maumbile.

Mapendekezo hayo yametolewa kwenye mkutano wa Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa, ulifanyika jijini Geneva, Uswisi.

Waziri wa Katiba na Sheria, Abdallah Ulega (katikati pichani), alieleza hayo katika mkutano huo, akieleza kwamba mapendekezo hayo ya Umoja wa Mataifa, ni kinyume cha mila, desturi, tamaduni na maadili ya jamii ya kitanzania.

"Tanzania haijaunga mkono mapendekezo yanayotaka kuhalalishwa kwa mahusiano ya jinsia moja, yakiwamo yanayotaka kuondolewa kwa adhabu kwa makosa ya kujamiiana kinyume na maumbile.

"Tunafanya hivyo ili kuzingatia sheria zilizopo pamoja na mila, desturi, tamaduni na maadili ya jamii ya kitanzania," alisema Ulega.

Msimamo huo ulikuwa ni sehemu ya wasilisho la Tanzania wakati wa kuwasilisha msimamo wake kuhusu mapendekezo yaliyotolewa katika mchakato wa Mapitio ya Hali ya Haki za Binadamu kwa Nchi (UPR) unaofanyika chini ya Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa.

Tanzania ilieleza kuwa haijaunga mkono jumla ya mapendekezo 68 kwa sababu mbalimbali, kama vile kutofautiana kwa baadhi ya misimamo ya kitaifa kuhusu masuala mahsusi, pamoja na hitaji la kufanya utafiti, tathmini na mashauriano zaidi kuhusu athari zake za kisheria, kisera, kijamii na kiuchumi.





CamScanner